HOTUBA YA JAJI MKUU MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA SIKU YA KUWAKUBALI MAWAKILI WAPYA KATIKA VIWANJA VYA UKUMBI WA KARIMJEE DAR ES SALAAM, TAREHE 14 DISEMBA, 2018

Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani,

Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Jaji Kiongozi,

Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu,

Profesa Adelardus Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

Biswalo Mganga, Mkurugenzi wa Mashtaka;

Wahe. Majaji Wastaafu wa Mahakama ya Rufani na wa Mahakama Kuu;

Wah. Msajili Mkuu, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Msajili wa Mahakama ya Rufani, Msajili wa Mahakama Kuu, Naibu Wasajili;

Mahakimu, Watendaji wa Mahakama, Wasaidizi wa Sheria wa Majaji na watumishi wote wa Mahakama;

Rais wa Chama Cha Wanasheria wa Tanganyika, Wakili Msomi Fatma Amani Karume;

Wasomi Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea;

Mawakili wapya pamoja na ndugu zenu, jamaa, marafiki na majirani zenu;

Mabibi na Mabwana.

AMANI YA MWENYEZI MUNGU, REHEMA NA BARAKA ZAKE ZIWAFIKIE NYOTE mliokusanyika hapa kushuhudia jumla ya mawakili wapya wapato 909 wakikubaliwa rasmi kuwa Mawakili wa Mahakama

Kuu ya Tanzania pamoja na Mahakama zilizopo chini ya Mahakama Kuu. KARIBUNI.

Ni safari ndefu, yenye changamoto nyingi hadi kufikia daraja la kukubaliwa kuwa WAKILI. Ni daraja ambalo, licha ya kutakiwa kuwa na uwezo mkubwa katika fani ya sheria, unatakiwa pia kuwa na uthabiti wa kimaamuzi na kujituma katika kila kazi za kisheria utakazofanya. Kwa niaba ya Mahakama ya Tanzania ningependa kuwapa mkono wa pongezi Mawakili wapya kwa kusafiri hiyo safari ndefu hadi kufikia kilele hiki cha mlima huu wa mafanikio katika taaluma ya Sheria.

Angalau kwa siku ya leo, kabla hamjaanza rasmi kazi, mnayo kila sababu ya kufurahi, kujipongeza, kupongezana, bila kusahau kumshukuru Mwenyezi Mungu, kuwashukuru wazazi wenu, waalimu wenu na wahadhiri, ndugu, jamaa, marafiki ambao bila shaka, wamekuwa na mchango mkubwa kwenu.

Kila Wakili ni Kiongozi katika Matumizi ya Sheria

Sina shaka yoyote kuwa kila mmoja wenu anafahamu umuhimu wa Sheria na pia nafasi ya Sheria katika maisha ya binadamu ambao wanaishi pamoja katika nchi kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Je? Mmewahi kujiuliza swali la kifalsafa la kwa nini kila nchi duniani ina

Sheria, na kwa nini kila nchi husisitiza umuhimu wa Utawala wa Sheria? Mwanafalsafa mmoja wa Uingereza, Thomas Hobbes, aliyeishi kati ya Mwaka 1588 na 1679 na ambaye nyote mnamfahamu; aliwahi kuuliza swali *"WHY DO LAWS EXIST?"* (kwa nini binadamu ana kuwa na Sheria?) Akajibu swali lake kwa kusema kuwa wanadamu hawawezi kuishi katika nchi kwa pamoja bila kuwa na Sheria. Alikumbusha hatari zilizokuwepo; enzi zile Mwanadamu alipokuwa akiishi katika zama zisizokuwa na Sheria—"*State of Nature, where everyone was entitled to do anything to anybody, this world would be war of all against all—and life would be nasty, brutish and short."* Mawakili wapya mkielewa umuhimu wa Sheria, kazi na Sheria na umuhimu wa kuzingatia Sheria, mtakubaliana na mimi kuwa mawakili ni watu muhimu sana katika jamii. Kazi zenu zinafungamana na umuhimu wa Sheria katika kuleta Amani na utulivu, kutoa nafasi kwa wananchi kustawi kijamii, kiuchumi, kisiasa na kimaendeleo kwa ujumla.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Sheria katika Nchi, kila Wakili ni kiongozi, ni mshauri, ni mtetezi na msimamizi katika kila jambo linaloratibiwa na kusimamiwa na Sheria. Nawaomba mtumie SHERIA kutatua na kumaliza migogoro Tumieni Sheria kuweka mazingira ya ustawi na maendeleo ya wananchi. Hakikisheni kuwa Sheria inakuwa

nyenzo wezeshi kwa wananchi ili waweze kufikia upeo wowote kulingana na stahili na uwezo wao.

Umuhimu wa daraja la UWAKILI utaliona leo katika sherehe ya kukubaliwa kwenu kujumuishwa katika orodha ya Mawakili. Baina yenu wapo wenye wadhifa na nafasi kubwa katika Jamii. Baadhi yenu ni Majaji wastaafu, Maprofesa wa Sheria, Maafisa Waandamizi wa Jeshi la Wananchi na Jeshi la Polisi. Wapo Wahadhiri, Mapadri, Mashekhe, bila kumsahau Balozi Mstaafu Tovako Manongi, mwana Diplomasia mahiri wa Tanzania aliyeacha sifa nyingi huko Umoja wa Mataifa.

Binafsi, nilipata nafasi adhimu sana, kwa mujibu wa kifungu 8(3) cha Sheria ya Mawakili, kukutana ana kwa ana na waombaji wa Uwakili wapatao 824. Kifungu hiki cha Sheria, kwa ujumla wake kinamtaka Jaji Mkuu ajiridhishe kuwa Wakili mtarajiwa ana sifa, ama tabia njema na anaufahamu wa kutosha wa lugha ya Mahakama – yaani Kiingereza na Kiswahili.

Licha ya kujiridhisha ufahamu na matumizi ya lugha ya Kiingereza, nilitumia muda huo kupima ufahamu wenu wa mambo yanayozunguka Sheria (General Knowledge), kuhusu Tanzania na kuhusu dunia inayozunguka Tanzania. Niseme kuwa, ufasaha katika kujieleza kwa lugha ya Kiingereza, bado ni changamoto inayotakiwa kufanyiwa kazi na

mfumo wetu wa elimu pamoja na Baraza la Sheria Tanzania, chini ya Mhe. Jaji Kiongozi. Mwalimu Nyerere aliwahi kutamka kwamba, "Kiingezeza ni Kiswahili cha Dunia". Kwa Wakili anayetaka kujifunza na kujiendeleza katika ushindani wa karne ya 21, hawezi kukwepa umuhimu wa kuwa na ufasaha katika lugha ya Kiingereza.

Changamoto kwa Mawakili wa Karne ya 21

Ingawa elimu yenu, kutoka shule za msingi, sekondari, vyuo kikuu na hata Elimu ya Sheria kwa Vitendo imejengwa katika misingi na maudhui ya karne ya 20, huduma za Uwakili mtakazotoa ni lazima zikidhi ushindani, na matarajio ya huduma za Karne ya 21.

Mtaweza tu kutoa huduma yenye ubora na ushindani stahiki kwa karne ya 21 kama mtajisomea maeneo mapya na kujiendeleza. Katika karne ya 21 "*Self-learning*" ni njia muhimu ya kujijenga na kujiendeleza kitaaluma kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, kutafuta kile unachotaka kusoma, na kusoma, kile unachotaka kusoma. Elimu kwa kujiendeleza inaongezea elimu tuliyozoea, kutoka juu kwa Wahadhiri na Walimu; hadi chini, kwa wanafunzi: "*You drive the learning process and this tends to be more effective than instructional learning.*"[1]

[1] **Be Your Own Teacher: Why And How Self-Learning Is Important,** https://www.brightermonday.co.ke/blog/self-learning/

Katika kujisomea na kujiendeleza, ningependa kuwasisitizia umuhimu wa kuelewa changamoto zinazoikabili nchi yetu Tanzania na kwa namna gani Sheria inaweza kusaidia kukabili changamoto.

Aidha, kila mmoja wenu ni lazima aelewe jitihada kubwa zinazofanywa na Mahakama ya Tanzania kukabiliana na changamoto zinazokabili utoaji haki. Mnayo jukumu kuyaelewa hayo maboresho. Maboresho makubwa yanaendelea kwa sasa ndani ya Mahakama ya Tanzania kupitia Programu za Maboresho na Mpango Mkakati wa Miaka Mitano ambayo imesaidia Majaji na Mahakimu kujipima kwa kupunguza milundikano ya mashauri. Maboresho yamefanikisha ujenzi wa majengo mapya ya Mahakama na kufanya ukarabati mkubwa. Aidha, Maboresho hayo yamejenga misingi ya kudumu ya kuwa na Mahakama itakayoendeshwa kwa uwazi na kwa kuzingatia Mifumo ya kisasa ya TEHAMA. Ni wajibu wenu Mawakili wapya kuwa sehemu ya maboresho na kuhakikisha kuwa huduma za utoaji haki zinakuwa karibu zaidi na wananchi *(Citizen-Centric)*.

Jitayarisheni kuwa sehemu ya mabadiliko ya sheria na kanuni za uendeshaji wa mashauri ziboreshwe na zieleweke kwa urahisi na ziharakishe utoaji haki. Kwa bahati mbaya, ipo mifano ya maboresho

yanayofanywa na Mahakama kukwama au kuchelewa kwa sababu tu Mawakili walio katika nafasi za utungaji sera wanakuwa hawajui mapana ya mwelekeo wa maboresho ya Mahakama.

Ubora ya Wakili huimarishwa na Uzingatiaji Maadili Mema

Kuboresha utoaji haki na utawala wa Sheria unategemea kwa kiasi kikubwa kuzingatiwa maarifa, weledi sambamba na maadili. Kama alivyosisitiza Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika, taaluma ya sheria ni taaluma yenye heshima (NOBLE PROFESSION), uwakili ni kazi inayohitaji kuaminiwa na kuaminika. Maadili mema na uwezo ni nguzo muhimu sana kwa ushindani wa huduma za kiwakili katika karne ya 21.

Kanuni Mpya Kusimamia Maadili, Nidhamu ya mawakili

Ili kuwasaidia Mawakili waendelee kuaminiwa na kuaminika, na wabaki ndani ya misingi ya Maadili na huduma bora za Uwakili, KANUNI ZA KIMAADILI, NIDHAMU NA TABIA NJEMA ZA MAWAKILI (*The Advocates (Professional Conduct and Ettiquette) Regulations, 2018 GN No. 118 of 2018*) tayari zimeanza kutumika mwaka huu. Kanuni hizi, zinawakumbusha mawakili mambo kadhaa ya msingi katika kazi za Uwakili. Vile vile zinatoa tahadhari kuwa hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa yeyote atakayekiuka hizi kanuni.

Nitatoa mifano michache ya miongozo kwa Mawakili iliyoletwa na Kanuni hizi.

Kanuni inasisitiza Uadilifu (*integrity*) unaotegemewa kutoka kwa kila Wakili. Wakili ni afisa wa mahakama mwenye tabia njema isiyo na dosari (*high moral principle).* Wakili ni mkweli, na atafanya kazi kwa kuheshimu misingi ya haki *(professional soundness of moral principle)*, unyoofu (*uprightness*), anayetoa huduma kwa dhati (*sincerity*) na kwa kuaminika (*trustfulness*).

Wakili anatakiwa kuwaheshimu wateja wake, wananchi, mawakili wenzake na wanasheria wenzake, na atawaheshimu pia wataalamu kutoka fani nyingine, bila kusahau kuiheshimu Mahakama na pia kuheshimu mfumo wa sheria na utoaji haki.

Kanuni zimeainisha mifano ya wakili ambaye atachukuliwa kuwa amekosa uadilifu na tabia njema—

- Wakili aliyevunja au kukiuka SHERIA za nchi:*fraud, making false returns, falsifying documents, portraying certain competence which he does not have)*;
- (ii) kuficha ukweli kwa wateja *(concealing material facts);*

- (iii) matusi, kusingizia, kutoa taarifa za uongo au maneno ya kudhalilisha maafisa wengine wa mahakama au viongozi wa umma. Kutoa taarifa za kupotosha *(fake news, loose-talk, rumours, gossips)*;
- (iv) matumizi mabaya ya fedha au mali za mteja.

Wakili anatakiwa kuonyesha tabia njema ndani ya Mahakama na hata nje ya Mahakama, hususan majumbani, sehemu za starehe au sehemu zingine nje ya mazingira ya kimahakama.

Wajibu wa Wakili kutoa Huduma Bora za Uwakili

Kanuni zinamtaka kila Wakili ana wajibu wa msingi wa kutoa huduma bora za kiwakili *(Quality service)*. Mahakama, wateja wenu, na mawakili wenzenu wana haki ya kudai na kutegemea huduma bora kutoka kwa kila mmoja wenu. Wakili ni lazima siku zote aonyeshe kuwa ana Maarifa ya kutosha, Ujuzi na uwezo wa kutosha kufanya kazi za kiwakili bila ubabaishaji.

Kanuni zimetoa mifano ya huduma mbovu zinazoweza kusababisha mawakili kuchukuliwa hatua za kinidhamu na hata kusimamishwa Uwakili:

- —(i) kushindwa kumpa mteja wako taarifa muhimu za maswala uliyoajiriwa kufanya;
- —(ii) kushindwa kutoa taarifa kwa mteja wako pale anapohitaji;
- — (iii) kushindwa kutoa huduma kwa sababu ya ulevi au matumizi ya dawa za kulevya au pombe;
- — (iv) kushindwa kuchukua hatua muhimu za kimahakama kwa niaba ya mteja wako na kusabisha kuchelewa kwa shauri au kusababisha gharama zisizo za lazima dhidi ya mteja wako. Mfano hapa ni pamoja na kushindwa kuandika barua ya kuomba nakala ya mwenendo wa mashauri ndani ya muda uliowekwa kisheria; au kushindwa kuwasilisha ombi au kutumia kifungu cha sheria au kanuni ambayo sio sahihi kwa jambo hilo: *(failure to respond, file replying pleadings, failure to write letters on behalf of client, occasioning delays or cost against the clients);*
- — (v) kutoa huduma mbovu, kwa mfano ubovu wa hati za kimahakama, kutayarisha hati za kimahakama zisizoeleweka, makosa ya kiufundi katika hati za kimahakama, zinazoweza kusababisha kesi kuondolewa au kufutwa na mahakama *(shoddy*

work, poorly drafted pleadings, mistakes, errors raising possibility of striking out of pleadings); na

- — (vi) kushindwa kuwa na ofisi ambazo wateja, mawakili wenzako na mahakama zinaweza kukufikia na kuwasilisha taarifa. Hivi karibuni, tutamtaka kila Wakili asajili eneo ilipo ofisi yake, mtaa na postikodi ili aweze kufikiwa.

Mawakili wote wanakumbuka maeneo yaliyotamkwa mwaka 1932 na Lord Macmillan katika kesi maarufu ya **DONOGHUE Vs. STEVENSON** – "**Categories of negligene are never closed**" - yaani mifano ya kesi za madai yatokanayo na uzembe hayana mwisho au kikomo. Kila Wakili, mpya au wa zamani, ni lazima akumbuke kuwa asipotoa huduma iliyo bora kulingana na mizani iliyowekwa na Kanuni, mteja wake anaweza kumshtaki mbele ya Kamati ya Nidhamu ya Mawakili (ADVOCATES COMMITTEE), au kumfungulia kesi Mahakamani kwa madai ya uzembe *(professional negligence)* kwa kutoa huduma chini ya kiwango kinachotarajiwa kutoka kwa Wakili wa kawaida au anaweza kufunguliwa kesi ya madai kwa kukiuka masharti ya mkataba *(contract)* kutoa huduma husika kiwakili.

Mwisho

Ningependa kumaliza hotuba yangu kwa kunukuu maneno yaliyosheheni busara, kutoka kwa Jaji **Mary E. Fairdshust** Jaji wa Mahakama ya Juu ya Jimbo la Washington huko Marekani mnamo mwezi Mei 2006 wakati wa Sherehe kama za leo, za kuwakubali Mawakili Wapya wa Jimbo hilo la Washington:[2]

> *"The law is a noble calling. Don't forget what our calling is about. It is not about winning or telling a client what he or she wants to hear. It is about making sure justice is done. It is about finding real solutions to real problems with the satisfaction that justice has also been served today and into the future. We enter this noble profession because we want to help people and solve problems. The justice system is our tool to do that. But we can't expect justice to prevail if we take it for granted.*
>
> *We have a choice. We have a responsibility. We can be stewards of justice who fight to ensure access, who are professional and civil at all times, who look for real solutions which will stand the test of time, and who will embrace changes to the practice of law which will enhance justice.*

[2] Justice Mary E. Fairhurst, "Welcoming Remarks to New Bar Admittees," Seattle Journal for Social Justice Vol. 4 Issue 2.

I know the course I have chosen. I am confident you will join me as you enter this noble profession…. Welcome."

Kwa haya machache, kwa niaba ya Mahakama ya Tanzania, ningependa kuwakaribisha sana kuwa Maafisa wa Mahakama. Nawatakia Siku Kuu Njema ya Krismasi, Mwaka Mpya na kuwatakia furaha na mafanikio katika majukumu yenu ya Uwakili katika Karne ya 21.

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA